

HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO

Barua zote ziandikwe kwa
Mkurugenzi Mtendaji Wilaya.
Simu No. 027-2539603/2
Fax: No. 027 - 2539603
Email: ded@longidodc.go.tz
Website: www.longidodc.go.tz



S. L. P 84,
LONGIDO,
MKOA WA ARUSHA.

KUMB.NA.HW/LONG/T/20/VOL.1/07

21.02.2022

TANGAZO LA AJIRA YA MUDA KWA VIJANA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido anapenda kuwatangazia nafasi za Ajira ya muda kwa vijana wote wenye sifa. Nafasi mia tatu (300) za wakusanya taarifa kwenye zoezi la Anwani za Makazi na Postikodi kata na vijiji vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Tangazo hili limefuta tangazo la tarehe 18.02.2022 lililo kuwa na KUMB.NA.HW/LONG/T/20/VOL.1/05

A: SIFA ZA WAOMBAJI

- i) Awe Raia wa Tanzania mwenye Umri wa kati ya miaka 18-35
- ii) Awe na elimu kuanzia Kidato cha Nne na kuendelea
- iii) Awe anamiliki simu janja Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima
- iv) Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayo fanya kazi
- v) Awe na uwezo wa kusoma Ramani
- vi) Awe ni Mkazi wa Kata husika

B: KAZI NA MAJUKUMU

- (a) Kugawa/kuandika Namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- (b) Kukusanya taarifa za Nyumba, Viwanja na maeneo ya huduma.

(c) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa Anwani za Makazi

(d) Kutumia Data kwenye mfumo wa Anwani za Makazi

C: MAOMBI YA AMBATANISHWE NA:

(i) Nakala ya cheti cha Kidato cha Nne na kuendelea

(ii) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa

(iii) Picha (Passport size)

D: MUDA WA AJIRA

Matarajio ya Ajira hii ya muda ni siku thelathini (30)


E: JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na Anwani Kamili ya muombaji, namba ya simu, Barua pepe na zipitie kwa Watendaji wa Vijiji na Kata anapoishi na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido kwa anwani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO,
S.L.P 84,
LONGIDO, ARUSHA**

F: TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25.02.2022 Saa 9.30 Alasiri


**STEPHEN A. ULAYA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO**